darasahuru.co.tz

**HALMASHAURI YA WILAYA YA ……….**

**MTIHANI WA MAJARIBIO YA NUSU MUHULA WA I DARASA LA V**

**SOMO: URAIA NA MAADILI**

**Muda: saa 1:30   Jina la mtahiniwa: Machi 2024**

**SEHEMU A: MASWALI YA KUCHAGUA (ALAMA 20)**

1. **Andika herufi ya jibu sahihi kwenye mabano uliyopewa** (Kila kipengele kina alama 1)

i Tunashauriwa tusikate miti ovyo na kuchoma misitu. Je, ni athari gani tunaweza kuipata tusipozingatia hayo? A. mifugo itakosa malisho B. kukosa eneo la kilimo C. ukame na baa la njaa D. watoto kupata elimu bora E. tutapata mvua nyingi na eneo kubwa la kilimo ( )

ii Kama mwanafunzi mwenzako amepatwa na tatizo unaweza kumfanyia yafuatayo isipokuwa: A. kumtenga B. kumpa pole C. kumshauri namna nzuri ya kutatua tatizo D. kumshika mkono E. kutoa taarifa kwa wazazi wake ( )

iii Mara nyingi watu huishi pamoja na kushirikiana katika shughuli mbalimbali. Je, watu hao huitwaje? A. binadamu B. jamii C. ukoo D. familia E. Shule ( )

iv Kuna njia mbalimbali za kupata viongozi mbalimbali ambazo ni uteuzi, uchaguzi na urithi. Je, kati ya viongozi wafuatao ni yupi huteuliwa? A. mwenyekiti wa serikali ya kijiji B. Diwani wa Kata C. mwalimu mkuu D. mbunge E. Mwenyekiti wa mtaa ( )

v Nani kati ya viongozi wafuatao ndiye katibu wa vikao vya baraza la Madiwani? A. Mkuu wa wilaya B. Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri C. Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya D. Katibu tawala wa wilaya E. Ofisa Elimu Wilaya

vi Ipi kati ya yafuatayo ni dalili ya mtu mwaminifu? A. kusema uongo B. kuwa mbinafsi C. kusaliti wenzake D. kusema ukweli E. wizi ( )

vii Rebeca ni mtoto wa miaka 9 lakini ana ufahamu juu ya mambo mengi sana na katika maisha yake haoni shida kumwambia mtu makosa yake pale anapokosea kufanya jambo fulani. Je, kitendo cha kuwambia mtu makosa yake huitwaje? A. kumuadhibu B. kumsimanga C. kumkosoa D. kumuonya E. Kumfundisha ( )

viii Makundi maalumu ya watu ni watu maalumu ambao wana uhitaji wa mahitajji mbalimbali. Yafuatayo ni makundi ya watu wenye uhitaji maalumu isipokuwa: A. watoto B. Wagonjwa C. Walemavu D. Wazee E. viongozi ( )

ix Miongoni mwa alama za taifa letu ni bendera ya taifa na bendera ya Rais. Je, bendera ya Rais ina rangi ngapi? A. 4 B. 3 C. 2 D. 1 E. 8

x Sehemu palipopakwa rangi za pundamilia katika barabara za lami matumizi yake ni yapi? A. kuegesha magari B. kupanda abiria C. kushuka abiria D. kivuko cha watembea kwa miguu E. kituo cha askari wa usalama

2. **Jibu kipengele (i) - (v) kwa kuoanisha maelezo kuhusu alama za Taifa katika fungu A na alama za Taifa au alama katika alama za taifa kutoka fungu B. Andika herufi ya jibu sahihi kwenye mabano.**

| FUNGU A | HERUFI | FUNGU B |
|---|---|---|
| 1. Huonesha utajiri wa mali asili ya nchi yetu. | ( ) | A. Bendera ya taifa |
| 2. Hutumika katika barua za kiofisi na machapisho ya serikali. | ( ) | B. Jembe na nyundo |
| 3. Huashiria uhuru wa nchi yetu. | ( ) | C. Ramani ya Tanzania |
| 4. Huwakilisha vifaa vinavyotumika kuendeleza taifa. | ( ) | D. Nembo ya taifa. |
| 5. Kutambulisha na kuonesha mipaka ya nchi yetu na nchi nyingine zilizo jirani yetu | ( ) | E. Fedha za Tanzania<br>F. Pembe za ndovu |

3. **Chagua neno au maneno kutoka katika kisanduku kukamilisha kipengele *i* hadi *v***

| |
|---|
| nne, kanzu na msuli, matusi, jinsia, kaptura nyeupe na shati jeupe, kijani |

i. ………………………… ni uhusiano uliopo kati ya mwanamke na mwanaume ulioundwa na jamii husika.

ii. Tendo mojawapo la udhalilishaji. ……………………………………………………………

iii. Mavazi ambayo huvaliwa wakati wa kucheza ngoma ya mganda. …………………………………..…..

iv. Mavazi ambayo huvaliwa na watu wa jamii za Pwani ……………………………………………………

v. Bendera ya Rais ina rangi ……………………………………………………………………………

**SEHEMU B: MASWALI YA MAJIBU MAFUPI** (ALAMA 20)

**4. Ufuataao ni muundo wa utawala katika kata. Kamilisha muundo huo kwa kutaja ngazi husika kwa kipengele *i* hadi *iv* ukianza na ngazi ya juu kabisa hadi ngazi ya chini.**

i. → ii. → iii. → iv.

Taja jina la kiongozi ambaye huongoza ngazi iliyooneshwa kwa namba **i**. ………………………………………

**5. Andika majibu sahihi katika nafasi uliyopewa.** (Kila kipengele kina alama 2)

i. Kumbukumbu ya siku ya Mapinduzi ya Zanzibar huadhimishwa tarehe …………………………………….…………… mwezi ……………………………….…………... kila mwaka.

ii. Jambo analostahili mtu kulipata bila kujali hali yake kama elimu kwa mtoto huitwa ……………………....

iii. Mkuu wa wilaya ni kiongozi mkuu wa serikali katika wilaya. Je, kiongozi huyu hupatikanaje? ……………………………………………………………………………………………………..


iv. Taja jukumu mojawapo la mwanafunzi awapo darasani. ………………………………………………………...

v. Jumla ya vitu vyote vinavyotuzunguka huitwa ………………………………………………………………...

**6. Chunguza picha zifuatazo kisha jibu maswali yanayofuata.**



**Picha namba 1**



**Picha namba 2**

**MASWALI**

i. Ni picha namba ngapi inaonesha tendo la usafi wa mazingira? ……………………………………………

ii. Ni kitendo gani kinachofanywa na wanafunzi hao kwenye picha namba 1? …………………………………

iii. Tendo la utunzaji wa mazingira linaoneshwa kwa picha namba ngapi? ……………………………………...

iv. Je, kuna faida gani ya kitendo kinachofanywa na wanafunzi kwenye picha namba 2? ……………………………………………………………………………………………………………

v. Taja faida moja tu ya kimazingira itokanayo na tendo linalofanywa na wanafunzi kwenye picha namba 1. ……………………………………………………………………………………………………………